# MKUTANO KATI YA IDARA YA WANYAMAPORI, JUMUIA ZA KIJAMII ZILIZOIDHINISHWA (AA) ZA MAENEO YA HIFADHI ZA WANYAMAPORI ZA JUMUIA (WMA), WAWAKILISHI WA VIJIJI, WILAYA NA MAKAMPUNI YA KITALII JUU YA KANUNI ZA UTUMIAJI WANYAMAPORI KATIKA ARDHI ZA VIJIJI NA MAENEO TENGEFU

**APRILI 28-29, 2008**
**HOTEL YA IMPALA, ARUSHA**

# KUMBUKUMBU ZA MKUTANO NA MAANGALIZO


**IMEANDALIWA NA:**
**JUMUIKO LA MALIASILI TANZANIA (TNRF)**
**SLP 15605, ARUSHA**
info@tnrf.org



**Washiriki wa mkutano na itifaki viliwezeshwa na:**
*Mfuko wa Wanyamapori Afrika (AWF)*
*Jumuiko la Maliasili Tanzania (TNRF)*
*Idara ya Wanyamapori, Wizara ya Maliasili na Utalii*

**Kwa msaada wa kiukarimu toka:**
**Hoteli ya Impala Ltd.**


**Kanusho:** Muhtasari huu si nakala halisi ya kumbukumbu za mkutano. Badala yake zinawakilisha hoja za msingi na masuala muhimu yaliyowasilishwa, yaliyochangiwa na kujadiliwa katika mjadala katika mkutano wa siku mbili na pia kama muhtasari wa mijadala katika vikundi.

# MUHTASARI MKUU

Mkutano huu uliitishwa na Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori kama sehemu ya kufungua ukurasa mpya katika mahusiano na ushirikiano kati ya Idara ya Wanyamapori na wadau wa wanyamapori – jamii, sekta binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali. Kwa ujumla takribani watu 350 walihudhuria katika mkutano wa siku mbili na hili ilitokana na ushirikiano mzuri miongoni mwa wawezeshaji wa mkutano.

Kanuni za Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (2005) ikilinganishwa na Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia yenyewe vilijadiliwa siku ya kwanza ya mkutano. Siku ya pili mkutano ulijadili na kutafuta maoni juu ya Kanuni za Uhifadhi wa Wanyamapori (Matumizi yasiyo ya uvunaji), tangazo la serikali na. 196 la tarehe 14 Septemba 2007 (Hapa imerejewa kama 'Kanuni Mpya').

Zaidi ya hapo, Uhifadhi Wanyamapori (Uwindaji Wanyama) Kanuni: Tangazo la Serikali Na. 272 (1974), Uhifadhi Wanyamapori (Ukamataji Wanyama) Kanuni: Tangazo la Serikali Na. 274 (1974) na Uhifadhi Wanyama (Uwindaji Kitalii) Kanuni: Tangazo la Serikali Na. 306 (2002) zilirejewa lakini hazikujadiliwa kwa undani kama Kanuni Mpya.

Mjadala kwa siku zote mbili ulikuwa wazi, huru na unakigusa kila nyanja, na uwakilishi mpana kutoka kwa wadau wote. Usimamizi wa mkutano siku ya pili ulikuwa mzuri zaidi ukilinganisha na siku ya kwanza. Kwa upande mwingine, hali ya mkutano siku zote mbili ulikuwa wa kujenga na mtazamo chanya. Mkutano ulipangwa katika hali ya kuimarisha mahusiano na mawasiliano kwa uwazi miongoni mwa Idara ya Wanyamapori na wadau wote na hivyo kuruhusu mawazo na mangalizo muhimu kutolewa.

Umakini wa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori ulimwezesha kuanza na migogoro iliyopo kati ya makampuni ya uwindaji na yale ya kupiga picha, na pia kati ya makampuni ya kitalii na wananchi. Baadhi ya masuala yalijadiliwa katika mkutano wa siku mbili, lakini zaidi katika mkutano maalumu wa wadau waliotoka Wilaya za Longido, Simanjiro na Serengeti na mkutano mwingine ambao ulikwishafanyika Wilaya ya Ngorongoro. Matokeo ya mikutano hiyo yameelezwa katika taarifa tofauti.

**A. Siku ya kwanza**

Wanajamii, wawakilishi toka halmashauri na mashirika yasiyo ya kiserikali walihudhuria siku hii. Pia makampuni machache ya wawindaji na wapiga picha nao walihudhuria. Baada ya mada ya maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Wanajamii, Usimamizi wa Ardhi na Kanuni Mpya makundi yalijadili mada zifuatazo:

1. **Mgawanyo wa mapato**
    - i. Mapato ni vyema yagawanywe kwa haki kudhiti migogoro.
    - ii. 35% ipewe serikali kuu
    - iii. 65% serikali za mitaa zinapata zaidi kwa sababu ziko karibu na migogoro ya wanyama.
    - iv. Serikali ya mitaa inatakiwa kupata 65% kwa sababu zifuatazo:
        - a. Jamii huathirika zaidi na wanyamapori
        - b. Raia wanaoishi na wanyamapori si rahisi kujihusisha na shughuli za uzalishaji kama ufugaji na kilimo.
    - v. Mara 65% ifikapo wilayani, 60% ipewe jamii na 40% itumiwe na shughuli za Halmashauri

2. ***Usimamizi wa vitalu vya uwindaji***
    - i. Maombi ya vitalu katika Mapori ya Akiba yapelekwe moja kwa moja kwa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori.
    - ii. Maombi ya vitalu katika Maeneo ya Hifadhi ya Jumuia (WMA) mara baada ya kujadiliwa yapelekwe katika Bodi ya Ushauri ya Wilaya na badae kwa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori kwa idhini yake.

iii. Ni wajibu wa Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa kufuatilia vitalu vilivyo katika Maeneo ya Hifadhi ya Jumuia (WMA).

**3. Utatuzi wa migogoro**

i. Njia za Utatuzi wa Migogoro
- Kila eneo liwe na mpango wa matumizi bora ya ardhi. Mpango huu ni budi uheshimiwe na kufuatwa na wadau wote.
- Kanuni, sheria na mchakato ni budi vifuatwe na makundi yote.
- Kama mgogoro ukijitokeza, utatuzi uanze na majadiliano miongoni mwa wahusika tu

ii. Kama majadiliano ya awali yameshindikana, wahusika waende kwenye Bodi ya Ushauri ya Wilaya katika maeneo ya hifadhi ya vijiji kwa ushauri zaidi.
- Na kama Bodi ya Ushauri ya Wilaya ikishindwa, basi, wahusika wachague msuluhishi ambaye anakubalika pande zote.
- Na kama msuluhishi akishindwa, wahusika wapeleke shauri lao mahakamani.
- Pia, mikataba ni budi ipitiwe mara kwa mara.
- Adhabu kwa mwekezaji anayevunja sheria iwe kubwa.

**B. Siku ya pili**

Makampuni ya sekta binafsi (hasa utalii wa kupiga picha na uvunaji) walihudhuria siku ya pili. Pamoja nao walihudhuria pia wawakilishi wachache toka jamii, halmashauri za wilaya na mashirika yasiyo ya kiserikali. Baada ya utangulizi wa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori na kuwasilishwa kwa mada ya Kanuni Mpya, vikundi vya mjadala vilijadili yafuatayo:

**1. Mfumo wa ada na utaratibu wa malipo**

i. Ilipendekezwa kuwa mfumo wa ada uliopendekezwa usitekelezwe. Unausumbufu, changamano, na hautekelezeki au kukagulika.

ii. Tunapendekeza mfumo wenye ngazi mbili ambao utawezekana na kutambua matakwa ya jamii na yale ya Idara ya Wanyamapori.
- ***Malipo ya 1: Ada ya kitanda***
  - a. Ada zitakubalika na mwenye kumiliki ardhi na mwekezaji (i.e. kijiji, Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa au idara ya wanyamapori)
  - b. Mikataba inabaki kuwa halali
- ***Malipo ya 2: Ada ya shughuli za Wanyama***
  - a. Ada hii hulipwa kwa Idara ya Wanyamapori na pia hujumuisha mchango wa wilaya.
  - b. Ada hii itajumuisha shughuli za kiutalii zilizoorodheshwa katika upiga picha wa kitalii.
    - Utalii wa picha (game drives)
    - Utalii wa picha – Usiku (night game drives)
    - Safari za miguu (walking safaris)
    - Milo nyikani (bush meals)
    - Mandari (picnics)
    - Safari za mitumbwi (rafting, boating)
    - Ada ya kuongoza wageni (guiding)

iii. Imependekezwa mfumo ufuatao wa ada (wasio wakJumuia ya Kijamii iliyoidhinishwazi):
- Mapori ya Akiba (GR) $30
- Mapori Tengefu (GCA) $15
- Maeneo ya Wazi / Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia $10
- Ada hizi hazitahusika: Ada ya gari, Ada ya kuongoza wageni, Ada ya kundi, Ada ya kiwanja, Ada ya mtumbwi

iv. Uvuvi inafikiriwa ni shughuli ya uvunaji.

v. Ada zisibadilishwe bila taarifa ya miezi 12.

vi. Makundi ya ada
- Wageni
- Wenyeji
- Watu wazima
- Watoto na wanafunzi

vii. Ulinzi wa eneo

a. Ada ya shughuli za wanyamapori inaweza kukusanywa na kulipwa kama mwekezaji ana makubaliano ya kulaza wageni na mmiliki wa radhi. Katika mapori ya akiba ada hiyo hulipwa Idara ya wanyamapori. Katika Mapori Tengefu and Maeneo ya wazi ada ya shughuli za wanyamapori hulipwa kijijini

b. Hii itasaidia watalii wa mchana tu kutoharibu raslimali na kuhimiza uwakili wa malihai.

viii. Hitimisho

a. Ada zote zikotolewe na kulipwa akaunti za benki Idara ya Wanyamapori au jamii

b. Malipo ya 1: Malipo ya kitanda tayari yapo.

c. Malipo ya 2: Yataombewa kuanzia Julai 1 2008 na kulipwa moja kwa moja kwa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori

d. Lengo ni kuunda mfumo rahisi ambao ni rahisi kuusimamia, rahisi kuukagua, ulio wazi, unaojitosheleza, endelevu, unaohakikisha wote jamii na serikali kuu wanafaidika na unalinda maliasili kwa vizazi vijavyo.

**2. Ni vipi watumia raslimali wote wanaweza kufanya kazi pamoja**

i. Wawekezaji wa utalii wa picha na uwindaji wanapaswa kufanya kazi kwa mwafaka.

ii. Chombo cha uratibu wa utalii wa picha na matumizi yasiyo ya uvunaji ni budi kiundwe ili kuhusisha makampuni yote ya utalii katika maamuzi.

iii. Wanavijiji, Maeneo ya hifadhi ya wanyamapori ya Jumuia na wawekezaji ni vizuri wawe wazi kwa masuala ya mchakato wa zabuni mikataba, majadiliano na makubaliano ya kimikataba.

iv. Mikataba katika maeneo ya Hifadhi ya Jamii inatakiwa kupanda hadi kuwa miaka 5 na mteja apewe nafasi ya kwanza katika kufanya upya mkataba kama ametimiza vigezo husika kiutendaji.

v. Hamasa ya wadau wa utalii ni vema iinuliwe hasa katika sera, sheria, kanuni na misingi ya biashara.

**3. Ugawanaji mafao na mapato**

i. Makundi husika:
- Jumuia ya Kijamii iliyoidhinishwa
- Wilaya
- Serikali kuu, Idara ya Wanyamapori
- Jamii

ii. Maeneo:
- Maeneo ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Jumuia (WMA)
- Mapori Tengefu
- Maeneo ya wazi
- Mapori ya Akiba

iii. Mapendekezo ya Mgawanyo:

a. Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) – Matumizi ya Uvunaji (Nyara) na Matumizi yasiyo ya Uvunaji.
   - Jamii 55 %
   - Wilaya 15 %
   - Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa 10 %
   - Idara ya Wanyamapori 20 %

b. Mapori Tengefu na Maeneo ya Wazi – Uvunaji (Nyara) na matumizi yasiyo ya uvunaji
   - Jamii 65 %
   - Wilaya 15 %
   - Idara wanyamapori 20 %

c. Mapori ya Akiba - haikujadiliwa.

**4. Nafasi ya watumiaji wa wanyamapori katika ulinzi wa raslimali**

Kuhakikisha uendelevu wa kiuchumi wa raslimali za wanyamapori kunahitajika:

i. Mawasiliano miongoni mwa wadau (yaani wawindaji, kampuni za kitalii, serikali, Asasi zisizo za kiserikali, jamii
ii. Ushirikiano miongoni mwa wadau wote
iii. Uwezeshaji
iv. Uwazi katika ngazi zote
v. Kushirikisha pande zote ili kupata mwafaka wa viunzi vya kisheria
vi. Urahisishaji na kunyoosha matendo ya kibiashara

## SHUKRANI

Jumuiko la Maliasili Tanzania (TNRF) na Mfuko wa Wanyamapori Afrika (AWF) wangependa kushukuru na kutambua ushirikiano uliotolewa na Idar ya Wanyamapori, hususa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori Bwana E. Tarimo, na Naibu Mkurugenzi, Maendeleo ya Wanyamapori, Bi. M. Zacharia waliowezesha mkutano huu ufanikiwe.

AWF na TNRF wangependa pia kutambua na kukiri msaada uliotolewa na Hoteli ya Impala katika kubeba baadhi ya gharama za kuendesha mkutano huu.

## YALIYOMO


1 UTANGULIZI ........ 9

2 SIKU YA KWANZA: JAMII ........ 10

2.1 Utambulisho kimakundi ........ 10

2.2 Sala ........ 10

2.3 Utangulizi kutoka kwa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori ........ 11

2.4 Mada juu ya Uwekezaji katika Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA), na Naibu Mkurugenzi, Maendeleo ya Wanyamapori, Bi. Miriam Zacharia ........ 11

Zifuatazo ni hoja zilizotolewa na ufafanuzi kutoka kwa mtoa mada: ........ 11

2.5 Mada juu ya Usimamizi wa Ardhi za Vijiji, na Bw. David Mushendwa, Mwanasheria, Wizara ya Ardhi, Makazi na Maendeleo ya Mijini, Ofisi ya Kamishina ........ 12

2.6 Mjadala wa Jumla ........ 13

2.7 Mada juu ya Kanuni za Uhifadhi wa Wanyamapori, Matumizi yasiyo ya Uvunaji (2007), na Kaimu Mkurugenzi, Matumizi ya Wanyamapori, Mr. Mohammed Madehele ........ 19

2.8 Mjadala kimakundi ........ 20

2.8.1 Mawasilisho juu ya mgawanyo wa mapato ........ 21

2.8.2 Mawasilisho juu ya mfumo wa ada ........ 21

2.8.3 Mawasilisho juu ya usimamizi wa vitalu vya uwindaji ........ 22

2.8.4 *A. Mapendekezo:* ........ 22

2.8.5 Mawasilisho juu ya Utatuzi wa Migogoro ya matumizi ya Raslimali ........ 22

3 MAKAMPUNI YA KITALII NA WAWEKEZAJI ........ 24

3.1 Utambulisho kimakundi ........ 24

3.2 Sala ........ 24

3.3 Utambulisho na Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori ........ 24

3.4 Mada juu ya "Kanuni za matumizi mbalimbali ya wanyamapori" na Kaimu Mkurugenzi, Matumizi ya Wanyamaporim, Bw. Mohammed Madehele ........ 25

3.5 Michango ya wote ........ 26

3.6 Mjadala kimakundi ........ 29

3.6.1 Mawasilisho1：Mfumo wa Ada na Utaratibu wa Malipo ........ 29

3.6.2 Mawasilisho 2: Ni vipi watumiaji wa raslimali wanyamapori wanaweza kukaa pamoja? ..... 30
3.6.3 Mawasilisho 3: Ugawanaji Mafao na Mapato ..... 31
3.6.4 Mawasilisho 4: Nafasi ya watumiaji wanyamapori katika ulinzi wa raslimali ..... 32
**3.7 Kufunga Mkutano ..... 33**
**A 1 Orodha ya Makabrasha Waliyopewa Washiriki ..... 34**
**A 2 Orodha ya Washiriki ..... 35**
**A 3 Muhtasari wa Tathmini ya Washiriki ..... 42**

# 1 UTANGULIZI

## MUHTASARI TENDAJI

Mkutano huu uliitishwa na Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori kama sehemu ya kufungua ukurasa mpya katika mahusiano na ushirikiano kati ya Idara ya Wanyamapori na wadau wa wanyamapori – jamii, sekta binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali. Kwa ujumla takribani watu 350 walihudhuria katika mkutano wa siku mbili na hili ilitokana na ushirikiano mzuri miongoni mwa wawezeshaji wa mkutano.

Kanuni za Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (2005) ikilinganishwa na Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia yenyewe vilijadiliwa siku ya kwanza ya mkutano. Siku ya pili mkutano ulijadili na kutafuta maoni juu ya Kanuni za Uhifadhi wa Wanyamapori (Matumizi yasiyo ya uvunaji), tangazo la serikali na. 196 la tarehe 14 Septemba 2007 (Hapa imerejewa kama 'Kanuni Mpya'). "Ingawa kulifanyika ushauri kidogo juu ya hali ya Kanuni Mpya, kwa ujumla Kanuni hizi zimewashangaza wengi na kusababisha hofu na mahangaiko"

Kwa muhtasari, Kanuni Mpya zinampa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori mamlaka juu ya matumizi yote ya utumiaji usio wa uvunaji nchini Tanzania. Hususani, Kanuni Mpya zinampa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori madaraka ya kuidhinisha au kusitisha matumizi ya biashara yoyote isiyo ya uvunaji wanyamapori katika maeneo nje ya hifadhi za taifa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. Zaidi sana, kanuni hizi zimeweka taratibu za kuombea vibali vya uendeshaji na kupanda ada zitakazotozwa kwa matumizi ya wanyamapori yasiyo ya ulaji ambazo zinapaswa kulipwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori.

Mkutano huu wa siku mbili ulijadili moja kwa moja masuala haya na kutoa mapendekezo ya kupitia mfumo wa ada wa sasa na kupanga kanuni za ugawanaji mapato.

Zaidi ya hapo, Uhifadhi Wanyamapori (Uwindaji Wanyama) Kanuni: Tangazo la Serikali Na. 272 (1974), Uhifadhi Wanyamapori (Ukamataji Wanyama) Kanuni: Tangazo la Serikali Na. 274 (1974) na Uhifadhi Wanyama (Uwindaji Kitalii) Kanuni: Tangazo la Serikali Na. 306 (2002) zilirejewa lakini hazikujadiliwa kwa undani kama Kanuni Mpya.

Mjadala kwa siku zote mbili ulikuwa wazi, huru na ukigusa kila nyanja, na uwakilishi mpana kutoka kwa wadau wote. Usimamizi wa mkutano siku ya pili ulikuwa mzuri zaidi ukilinganisha na siku ya kwanza. Kwa upande mwingine, hali ya mkutano siku zote mbili ulikuwa wa kujenga na mtazamo chanya. Mkutano ulipangwa katika hali ya kuimarisha mahusiano na mawasiliano kwa uwazi miongoni mwa Idara ya Wanyamapori na wadau wote na hivyo kuruhusu mawazo na maangalizo muhimu kutolewa.

Umakini wa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori ulimwezesha kuanza na migogoro iliyopo kati ya makampuni ya uwindaji nay ale ya kupiga picha, na pia kati ya makampuni ya kitalii na wananchi. Baadhi ya masuala yalijadiliwa katika mkutano wa siku mbili, lakini zaidi katika mkutano maalumu wa wadau waliotoka Longido, Simanjiro na Serengeti na mkutano mwingine ambao ulikwishafanyika awali huko Ngorongoro. Matokeo ya mikutano hiyo yameelezwa katika taarifa tofauti.

# 2 SIKU YA KWANZA: JAMII

**Kulingana na aina ya washiriki waliohudhuria siku ya kwanza mkutano uliendeshwa kwa Kiswahili.**

**Angalizo la Sekretariat ya TNRF:** Kwa ujumla, mkutano ulionekana kuwa umefanikiwa kwa vile uliweka msingi kwa mikutano ya ushauri kama huu hapo baadae. Hata hivyo, kwa dharura mkurugenzi alilazimika kuondoka kwa kwa siku ya kwanza. Mkutano ungeweza kufanyika vizuri na kusingekuwa na upotevu wa muda uliojitokeza siku ya kwanza kutokana na mwenyekiti wa siku hiyo. Uwezeshwaji wa baadhi ya kazi za vikundi ungekuwa umeboreshwa zaidi, hata hivyo kuna matokeo mazuri yalipatikana. Mkutano uliongozwa na Mkuu wa Wilaya na akiwa na wakuu wengine wa wilaya au wasaidizi wao pembeni yake; hii ilisababisha wakati fulani mkutano kuanza kuwa wa kisiasa na hivyo kupoteza mwelekeo wake kitaalamu na kutokuwa shirikishi vya kutosha kama ulivyotegemewa. Hata hivyo kuna baadhi ya matokeo mazuri yalipatikana. Pia, idadi ya wanavijiji, jumuia za kijamii zilizoidhinishwa na uwakilishi wa wilaya ulikuwa mkubwa.

## 2.1 Utambulisho kimakundi

**Washiriki:** (Kutoka Wilaya za  Babati, Serengeti, Mbulu, Monduli, Loliondo, Longido na Simanjiro)

- Viongozi wa jamii
- Viongozi wa Jumuia za kijamii ziliozoidhinishwa (AA) kuendesha Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA)
- Makatibu Tarafa
- Wakuu wa wilaya
- Viongozi wa CCM

- Mashirika yasiyo ya kiserikali: UCRT, PINGO, TAPHGO, Mfuko wa Wanyamapori Afrika (AWF), Jumuiko la Maliasili Tanzania (TNRF), WWF

- Idara ya Wanyamapori

**Wengine:**

- Makampuni ya uwindaji
- Makampuni ya utalii wa kupiga picha

## 2.2 Sala

Sala zilifanywa na baadhi ya watu baada ya kuombwa na Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori kufanya hivyo kutoka kwa madhehebu tofauti ya kiimani.

## 2.3 Utangulizi kutoka kwa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori

Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori alitoa ukaribisho kwa hotuba iliyowahimiza washiriki kuchangia kwa bidii katika majadiliano na kufikiri kwa makini juu ya maendeleo halisi dhidi ya Kanuni Mpya. Baada ya hapo Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori aliondoka kwa majukumu muhimu na akamchagua Mkuu wa Wilaya ya Babati, Bw. David Hollela kuongoza mkutano. Waandishi wa habari waliombwa kuhudhuria siku ya pili ili siku ya kwanza wananchi wawe huru kutoa mawazo yao bila woga wa kuwa kuna mtu anayechukua taarifa zao.

## 2.4 Mada juu ya Uwekezaji katika Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA), na Naibu Mkurugenzi, Maendeleo ya Wanyamapori, Bi. Miriam Zacharia

Zifuatazo ni hoja zilizotolewa na ufafanuzi kutoka kwa mtoa mada:

a. Kwanini kuwekeza katika Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA)?
b. Sera ya wanyamapori iliyorekebishwa (2007) haina tofauti sana na ile ya sera ya wanyamapori ya 1998. Kanuni Mpya (2007) zinaakisi masuala ya umiliki kutoka katika Sera ya Ardhi ya 1994. Hakuna chochote kinachohusiana na usimamizi wa wanyamapori kilichobadilika.
c. Hakuna sheria mpya ya wanyamapori hadi wakati huu, isipokuwa Kanuni Mpya.
d. Hakuna kanuni zingine mbali na Kanuni za Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) ambazo ndizo zitasimamia masuala ya wanyamapori katika ardhi ya vijiji.
e. Istilahi za usimamizi wa wanyamapori ni vizuri ziwe wazi. Mtu asiseme "*uendeshaji*" kumaanisha "*usimamizi*" akirejea kazi za kawaida za uendeshaji zinazofanywa na wanavijiji wakati neno hilo hutumiwa kumaanisha majukumu ya kiuendeshaji kiserikali zaidi.
f. Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) hayasimamiwi na serikali za vijiji, badala yake ni Jumuia za kijamii ziliyoidhinishwa (AA) ambazo ni Jumuia za Kijamii zinazoundwa na watu wazima waliozidi umri wa miaka 18, na kukubaliwa na serikali za vijiji kusimamia raslimali wanyamapori.
g. Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) haina mamlaka juu ya serikali ya kijiji kuhusiana na masuala ya ardhi. Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa ni wakala tu aliyeundwa ili kuendesha usimamizi wa wa wanyamapori.
h. Watu wanashangaa ni kwa nini viongozi wa Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) hawawezi pia kuwa wajumbe wa serikali ya kijiji. Sababu ni kwamba mtu akiwa na majukumu katika kila asasi anaweza kusababisha migongano ya kimasilahi. Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa si kwa faida ya wachache, bali ni kwa faida ya raia wote.
i. Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) yaweza kuingia katika mkataba na wawekezaji kwa matumizi ya wanyamapori katika ardhi ya kijiji. Mikataba hii yaweza kudumu miaka mitatu kabla ya kufanywa upya. Kipindi hiki kifupi hupunguza mzigo kwa jamii juu ya uwezekano wa kutokea migogoro kati ya wananchi na mwekezaji.
j. Marufuku kuunda mkataba kati ya Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) na kampuni ya uwindaji. Uwindaji unasimamiwa na Kanuni za Wanyamapori za 2000 pitio la 2002 (Uwindaji wa kitalii), na hivyo kuwa chini ya madaraka ya Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori.
k. Tathmini ya Athari za Mazingira (EIA) ni sharti la Baraza la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Sheria ya Usimamizi wa Mazingira (2004) na mwekezaji lazima alipie tathmini hiyo. Ni

vyema Halmashauri za Wilaya zielewe majadiliano ya kiuwekezaji ili ziweze kusaidia katika tathmini.

l. Serikali kuu ipo kwa ajili ya kutoa ushauri wa kitaalamu, lakini Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) itafanya kazi kwa karibu na mamlaka ya serikali ya mtaa.
m. Nafasi ya serikali kuu ni kufuatilia.
n. Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa huchagua maeneo ya makambi pamoja na uandaaji wa mpango kabambe wa uendeshaji wa eneo la hifadhi ya Jumuia (GMP au RZMP). Wawekezaji lazima wafuate maamuzi ya Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA), ambazo huhusisha masuala kama usimamizi wa maji, ikolojia ya wanyamapori na mahitaji ya mifugo.
o. Kumbuka kuwa jumuia za kijamii (CBO) na asasi zisizo za kiserikali (NGO) ziko chini ya mamlaka ya Mkuu wa Wilaya.
p. Kanuni za Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) pia hutoa viwango kwa mikataba ya uwekezaji.
q. Bodi ya Ushauri ya Wilaya kwa ajili ya Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) ina wawakilishi mbalimbali.
r. Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori lazima ajulishwe kuhusu mikataba hiyo.
s. Hakuna mwekezaji yeyote anayeweza kuingia katika eneo na kuanza kazi bila kutajwa katika mkataba.
t. Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) na mwekezaji lazima kwanza washauriane na Halmashauri za Wilaya kabla ya kuanza majadiliano yao. Na mkataba lazima uidhinishwe na wilaya. Hii inawagusa makampuni ya utalii wa kupiga picha.
u. Afisa Wanyamapori wa Wilaya katika mazingira fulani aweza kuwa ametoa vibali na hii atakuwa amefanya kimakosa. Hilo haliko ndani ya uwezo wake kutoa vibali katika maeneo ya Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA).
v. Maeneo ni vizuri yakagawanywa kikanda kulingana na matumizi ili kupunguza migogoro.

## 2.5 Mada juu ya Usimamizi wa Ardhi za Vijiji, na Bw. David Mushendwa, Mwanasheria, Wizara ya Ardhi, Makazi na Maendeleo ya Mijini, Ofisi ya Kamishina

1. Malengo ya mada ilikuwa ni kujibu maswali yafuatayo:
   a. Ni vipi ardhi inasimamiwa?
   b. Ni vipi ardhi ya kijiji inasimamiwa, na nani?
   c. Ni taratibu zipi za kisheria za kupata ardhi?
   d. Kuna tofauti gani kati ya usimamizi wa ardhi na ule wa maliasili?
2. Sera ya Ardhi ya 1995: Ardhi inasimamiwaje?
   a. Sheria zinazohusiana:
      i. Sheria ya ardhi (1999)
      ii. Sheria ya ardhi ya kijiji (1999)
   b. Ardhi imegawanywa katika mafungu matatu:
      iii. Ardhi ya Jumla – Chini ya Kamishina wa Ardhina ni mali ya Watanzania wote
      iv. Ardhi ya kijiji – Chini ya Halmashauri za wilaya
      v. Ardhi iliyohifadhiwa – inasimamiwa na sheria zifuatazo, kulingana na aina ya ulinzi unaotolewa: Sheria ya Hifadhi za Taifa, Sheria ya Mamlaka ya Ngorongoro, Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sheria ya Baraza la Mazingira, nk.

3. Ardhi ya kijiji inamilikiwaje? Na nani?
    a. Matumizi ya ardhi ya kijiji yanaweza kuhusisha kilimo na ufugaji.
    b. Ardhi iko chini ya mamlaka ya serikali ya kijiji, ambayo inakuwa kama mdhamini kwa niaba ya kijiji.
    c. Kila matumizi ya ardhi kijijini lazima yafanywe na serikali ya kijiji.
    d. Halmashauri za vijiji ni lazima:
        i. Kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya na kutekeleza miongozo kutoka Halmashauri ya Wilaya
        ii. Kushirikiana na Kamishina wa Ardhi kuratibu uwekezaji katika ardhi za vijiji.
        iii. Wawekezaji wa nchini na wa nje ambao sio serikali ni lazima wapitie kwa Kamishina wa Ardhi na kisha kutoa taarifa kwa Halmashauri ya Wilaya husika.
4. Ni taratibu zipi za kisheria za kupata ardhi?
    a. Serikali za vijiji zina uwezo wa kutoa vibali hadi hekta 20.
    b. Kutoka hekta 21-50 Halmashauri ya wilaya lazima itoe kibali.
    c. Kwa zaidi ya hekta 50, serikali ya kijiji lazima kupata kibali toka kwa Komishina wa Ardhi.
    d. Rejea kifungu na. 19-20 cha Sheria ya Ardhi (1999) na kifungu 18-21 cha Sheria ya Kijiji (1999).
    e. Ni Watanzania tu wanoruhusiwa kumiliki ardhi. Raia wasio Watanzania wanaweza tu kumiliki ardhi kwa ajili ya uwekezaji kama taasisi au biashara. Watu binafsi wasio Watanzania hawaruhusiwi kumiliki ardhi.
    f. Kituo cha Uwekezaji cha Taifa (TIC) huhusika na umiliki wa ardhi kwa wawekezaji wa kigeni. Serikali ya kijiji lazima ipate kibali (kwa niaba ya mwekezaji) kutoka kwa Kamishina wa Ardhi ili kuanzisha mchakato.
5. Kuna tofauti gani kati ya usimamizi wa ardhi na ule wa maliasili?
    a. Maliasili si sehemu ya ardhi, ingawa ziko juu au ndani ya ardhi. Ni vyema kutofautisha kati ya ardhi na maliasili zingine.
    b. Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) yametengwa kwa usimamizi wa raslimali wanyamapori katika ardhi ya kijiji.
    c. Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) ni chombo kilichoundwa kusimamia Maeneo ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Jumuia (WMA).
    d. Wanyamapori wako chini ya mamalaka ya Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori, katika Wizara ya Maliasili na Utalii.
    e. Vifungu 63ii na 63iii vya Sheria ya Ardhi ya Vijiji huhusu usimamizi wa ardhi ya kijiji.

## 2.6 Mjadala wa Jumla

Baada ya kuwasilisha mada, Mwenyekiti alifungua mjadala na ufafanuzi kwa washiriki. Baada ya kusikiliza maoni yote Naibu Mkurugenzi, maendeleo ya Wanyama alijibu maoni mengi akisaidiwa na na Bw. Mushendwa (toka ofisi ya Kamishina wa Ardhi) na Mwenyekiti. Si maswali yote yalijibiwa moja kwa moja kutokana na ukubwa wa mkutano na kwa sababu moja ya kusudi la mkutano lilikuwa kuandaa majibu kupitia maswali yanayoulizwa.

***Maswali kutoka ukumbini kwa watoa mada wote yaliunganishwa pamoja na kunukuliwa na watoa mada na baadae waliyajibu kwa pamoja pia. Maelezo yafuatayo yameandaliwa na Sekretariet ya TNRF ili kuwianisha majibu na maswali yaliyoulizwa.***

1. **Swali (Mwakilishi toka Babati):** Ni nini nafasi ya Baraza la Ardhi la Kata? Nani anatakiwa kuitisha mkutano wa Bodi ya Ushauri ya Wilaya (ya WMA)?

   **Jibu:** Vijiji hutuma watu 3-5 katika *Baraza la Ardhi la Kata kutegemeana na ida*di ya vijiji katika kata husika. Na kila Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) hupeleka wawakilishi katika Bodi ya Ushauri ya Wilaya.
2. **Swali (mwakilishi toka Wilaya ya Ngorongoro):** Kwa nini wawekezaji katika Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) huhitaji idhini ya Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori katika masuala fulani, tena kutoka kwa Kamishina wa Ardhi katika masula mengine wakati serikali ya kijiji wana mamlaka kamili katika ardhi ya kijiji? Ni nani huamua juu ya mgawanyo wa mapato kutoka Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA)?
   **Jibu:** Kwa sababu uwekezaji unahusiana na wanyamapori, Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori lazima aarifiwe maana ndio mwenye dhamana. Itakuwaje kama kampuni ya uwindaje itakuja tu na kibali toka kwa Waziri? Kampuni ni lazima ifuate taratibu za vijiji. Kwa kuzingatia migogoro ya ardhi bila shaka serikali za mitaa zilikosea tafsiri ya Sheria ya Ardhi ya Vijiji. Wote tunatumia raslimali, hivyo hakuna taasisi moja ambayo ni muhimu kuliko nyingine.
3. **Swali (Kampuni ya uwindaji):** Je wanyamapori ni mali ya Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) tu au mali ya Watanzania wote?

   **Jibu**: Wanyamapori ni mali ya umma. Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori amepewa uwakili au udhamini tu. Wanyamapori ni kwa Watanzania wote.
4. **Swali (Diwani, Wilaya ya Babati):** Kama vijiji wamepewa hati miliki ya ardhi, nani ni mmiliki wa wanyamapori?

   **Jibu:** Mmiliki ni serikali, kwa sababu wanyamapori ni mali ya umma na hawamilikiwi na mtu binafsi, kikundi au taasisi.
5. **Swali (Kampuni ya Utalii):** Nani ambaye mwekezaji wa utalii wa uwindaji atasaini nae mkataba kwa eneo ambalo ni Hifadhi ya Wanyamapori ya Jumuia, lakini uwekezaji unawekwa nje ya Eneo la Hifadhi ya Wanyamapori ya Jumuia (WMA) ? Itakuwaaje kama Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) iko chini ya vijiji vingi? Mkataba unakuwaje katika Maeneo ya Wazi?

   **Jibu:** Vitalu vinasimamiwa tofauti na Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA).
6. **Swali (Mwakilishi kutoka asasi za wafugaji):** Je uwekezaji wa aina tofauti unaweza kuwa katika eneo moja la Hifadhi ya Wanyamapori ya Jumuia (WMA)?

   **Jibu:** Uwekezaji wa aina tofauti unaruhusiwa ndani ya mipaka ya Mpango wa Matumizi ya Ardhi na Mpango Kabambe wa uendeshaji Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) (General Management Plan [GMP] or the interim Resource Management Zone Plan [RZMP]). Mpango huu huelekeza nini na nini kisifanyike. Hii ina maana kwamba matumizi tofauti yaweza kutekelezwa katika kanda ama msimu tofauti wa mwaka. Kanda hizi zitaruhusu matumizi ya uvunaji na yale yasiyo ya uvunaji, ambayo yatatofautiana kwa kutegemeana na mahali au msimu.
7. **Swali:** Nani anatakiwa kugharimikia uharibifu wa wanyamapori katika Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA)?

   **Jibu:** Upo mpango katika mchakato wa kushughulikia suala la fidia. Kabla ya uwekezaji wawekezaji wanatakiwa kulipia gharama za kufanya Tathmini ya Athari za Kimazingira. Ni vizuri Tathmini ya Athari za Kimazingira ikaweka pia masuala ya maji.

   **Angalizo la Sekretariet ya TNRF:** Mjumbe mmoja alishauri kwamba serikali ingefaa kuwa na watalaamu wake wa tathmini ya athari za kimazingira ili kuwa na tathmini ya ndani kuepuka upendeleo unaoweza kufanywa na watalaam wanaolipwa na wawekezaji wenyewe.

8. **Swali:** Mapato yakipatikana toka Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA), nani hulipwa moja kwa moja na mgawanyo unakuwaje?
   **Jibu:** Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) hawatakiwi kuihoji serikali ya kijiji juu ya matumizi ya mapato. Kuna mchakato uliopangwa wa kuwakilisha taarifa katika wilaya.
9. **Swali:** Nini tofauti ya kumiliki ardhi na kumiliki raslimali katika ardhi?
10. **Swali:** Nini hadhi ya Mapori Tengefu mahali vijiji vilipojengwa?
    **Jibu:** Serikali ipo katika mchakato wa kutengua Mapori Tengefu (GCA) ili kuruhusu vijiji kuomba wapewe hadhi Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA). Huu ni mchakato mrefu.
    **Jibu (Mwanasheria, Kamisheni ya Ardhi):** Unapobadilisha matumizi ya Ardhi, upande unaotaka Ardhi hubadili (mf. kutoka Pori tengefu kwenda Ardhi ya Kijiji) lazima aanzishe mchakato. Rais lazima aidhinishe badiliko hilo.
11. **Maoni (kampuni ya uwindaji)**: Kifungu cha 22 (maombi ya umiliki ardhi kimila *(Hati ya miliki ya kimila*) na Kifungu cha 23 (*Utafutaji wa Hati Miliki ya Kimila*) cha Sheria ya Ardhi (1999) hurejea tu kwa umiliki wa kimila wa ardhi na sio hati miliki ya kuridhia.
    **Jibu (Mwanasheria, Kamisheni ya Ardhi):** Kuna mchanganyo katika neno "hatimiliki" ambalo huweza kumaanisha kimila ama hati zingine zinazotolewa za umiliki wa ardhi.
12. **Maoni (Mkuu wa Wilaya, Ngorongoro):** Uwekezaji wa wageni una mchakato tofauti. Uwekezaji wao lazima upitie Kituo cha Uwekezaji cha Kitaifa (TIC)
13. **Maoni (Mwanasheria):** Alitoa maangalizo yafuatayo:
    a. Sio sehemu ya sheria kuwa Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) lazima iwajibike kwa Halmashauri ya Wilaya. Kanuni za Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) hazitamki waziwazi juu ya nafasi ya Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) na wilaya zaidi ya kusema Bodi ya Ushauri ya Wilaya itatoa ushauri kwa Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) katika Halmashauri ya Wilaya pamoja na kazi zingine zitakuwa kiungo kati ya Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) na Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori.
    b. Kifungu cha 70 (Makosa na adhabu) cha Kanuni za Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) ni hatari kwa sababu ni rahisi kwa wanavijiji kukosea na kuingia katika tatizo la faini. Hii inawaweka wananchi katika mtego wa kushitakiwa kirahisi kwa kushiriki kwa hiari katika shughuli za kijamii za uhifadhi wa wanyamapori.
    c. Je, Ardhi ya Jumla huhusu ardhi iliyopimwa au ile isiyopimwa? Baadhi ya maeneo ya majaribio ya Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) bado hayako chini ya mamlaka ya vijiji kama vile katika eneo la wilaya ya Ngorongoro, ambayo ina Pori Tengefu (GCA) katika Ardhi ya Kijiji.
       Ili Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) yaanzishwe, sharti ni kwamba Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) lazima yawe kwenye Ardhi ya Kijiji ambayo lazima itanguliwe kutoka ardhi iliyohifadhiwa. Katika maeneo mengine (mf. Wilaya za Ngorongoro, Babati, Monduli na Longido) kuna eneo ambalo ni ardhi ya kijiji na pia ni pori tengefu. Ardhi ya kijiji na ile ya pori tengefu vinaingiliana. Hali hii ni kinyume na Kanuni za Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) kwa maana Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) yameanzishwa katika maeneo yaliyohifadhiwa. Kuna tanbihi katika Kanuni za matumizi ya wanyamapori ambapo pamewekewa nyota. Nyota hiyo inasomeka; maeneo haya yasianzishwe kuwa Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) hadi pale ardhi itakapotenguliwa kutoka ardhi iliyohifadhiwa kwenda ardhi ya kijiji. Lakini hata leo hii hakujatokea habari kuwa waziri mwenye dhamana anaanzisha mchakato huo.

d. Je kijiji chaweza kuwa na Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) kwa chenyewe? Ndio, kama ni eneo muhimu kwa uendelevu wa kiikolojia.
e. Baadhi ya Jumuia za kijamii ziliyoidhinishwas zilianzishwa (AA) bila mikataba kutoka serikali za vijiji. Mikataba ya Jumuia za kijamii ziliyoidhinishwa (AA) wakati mwingine haikamilishwi.
f. Ufafanuzi wa "haki za kutumia" katika Kifungu cha 22A cha Kanuni za Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) (2005) kinachanganya: Napenda kutahadharisha wajumbe kuwa katika muktadha huu "haki za kutumia" inarejea katika haki ya kutumia raslimali wanyamapori katika Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA). Haki hizi za kutumia hutolewa na Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori. Haki hizi za kutumia mara nyingi huchanganywa na "haki za kutafutwa," au haki zisizo za asili ambazo ni masuala ya ardhi, hutolewa na serikali ya kijiji. Ni vizuri watu wakaelewa kuwa mamlaka ya halmashauri ya kijiji na Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwas ni tofauti kabisa. Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) iko chini ya uelekezi na ushauri wa serikali ya kijiji ili kushughulikia wanyamapori. Serikali ya kijiji ya kila Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) huwa na wawakilishi katika Meneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA).
g. Masharti muhimu mawili katika kifungu cha 22 cha Kanuni za Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) (2005) inahusisha makubaliano kati ya Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) na halmashauri ya kijiji. Kifungu 22B husema Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) haiwezi kuwa na mamlaka hadi kwanza imeingia katika makubaliano na halmashauri ya kijiji (yaani mkataba wa usimamizi) ambako halmashauri ya kijiji huipa Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) majukumu ya kusimamia Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) katika vijiji. Katika ukamilishaji makubaliano haya, kifungu cha 22J husema kuwa kila mwenye uwezekano wa kuwekeza katika Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) ni lazima itoe maombi kwa niaba ya mwekezaji katika mkutano wa hadhara kijijini kwa sehemu ya Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) ili kupewa kibali. Kijiji cha Rubanda eneo la Ikona kama eneo la Hifadhi ya Wanyamapori ya Jumuia (WMA) ni mfano wa mkataba wa usimamizi kati ya Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) na serikali ya kijiji ambao haukumaliziwa na uwekezaji unaendeshwa kati ya mwekezaji na Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) bila Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) kwanza kupeleka maombi na kupatiwa kibali kutoka mikutano ya hadhara ya vijiji husika.
h. Mara nyingi Bodi za Ushauri wa Wilaya kwa Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) sio hai.

14. **Maoni (mwakilishi wa Ngorongoro):** Mapori Tengefu (GCA) hayatakiwi kuwa karibu na vijiji. Ni sheria ipi inatawala ? Hii inasababisha matatizo mengi.
15. **Maoni (Mwakilishi kutoka Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa** (AA) **Ikona Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia WMA):** Tunahitaji tathmini ya Kanuni. Hii inaonekana inatoka juu. Matakwa binafsi ya Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori yanaweza kuathiri usimamizi. Nani mwangalizi? Ni vyema kuwashirikisha wadau.
16. **Maoni:** Mkataba wa uwekezaji ni vizuri uwe kwa kipindi cha miaka mitano. Uwekezaji na umiliki wa ardhi hautoi haki. Tathmini ya athari ya kimazingira huchukua muda kwa vile mwekezaji ndio anapaswa kulipa. Hii ingekuwa kazi ya serikali na sio jukumu la mwekezaji binafsi. "*Anayelipa ndiye anachagua muziki,*" Tunahitaji kuelezea pia uwindaji wa wazawa.
17. **Maoni (Ngorongoro Community member:** Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori anatakiwa awe na huruma. Je, Kanuni hufuata ilani ya CCM (2005-2010) ambako inasema wananchi wanapaswa kusimamia wanyamapori?

18. **Maoni (Mwakilishi toka Babati):** Halmashauri zavijiji hazipewi tena “Hatimiliki ya ardhi.” Badala yake wanapewa “Cheti cha ardhi ya vijiji.” Itakuwaje kama kuna vijiji viwili na kijiji kimoja kina ardhi zaidi katika Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA)? Nani atafaidi zaidi?
19. **Maoni (Ngorongoro):** Msituache nyuma. Kanuni zimejadiliwa tu katika ngazi ya wadau wa juu.
20. **Maoni (Mwenyekiti):** Usiseme hivyo kwa sababu tupo hapa leo kuzungumza nanyi.
21. **Maoni (Asasi ya wafugaji):** Si vema kuona baadhi ya vijiji wanalazimishwa kuingia katika Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA). Ni vipi uhuru wa vyama huria? Je haipaswi kuwa Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) – iwe asasi huru isiyo ya kiserikali - ikiwa chini ya sheria ya asasi zisizo za kiserikali?
22. **Swali:** nani anawajibika kwa nani: Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) na serikali ya kijiji? **Jibu:** Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) wamedhaminiwa na serikali ya kijiji ili kusimamia raslimali wanyamapori. Kwahiyo, Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) huwajibika kwa serikali za vijiji.
23. **Maoni:** Kifungu 70 cha Kanuni (makosa na adhabu) kipitiwe upya kwa sababu kinawaweka wananchi katika mtego na kwa vile dhana hii ni bado mpya na makosa ya kushitakiwa yanaweza kutendwa kirahisi.
24. **Angalizo la Sekretariet ya TNRF:** Maoni haya yalipokelewa kwa nguvu sana na wajumbe.
25. **Maoni (Kampuni ya uwindaji):** Mara nyingi wajumbe wa Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) husababisha ionekane kuwa Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) ni asasi yao binafsi.
26. **Maoni (Kampuni ya utalii):** Kama hatutatafuta ufumbuzi wa kudumu juu ya usimamizi wa wanyamapori, wageni wa nje watasafirisha wanyama wote kwenda nje. Si haki kuona mgeni mmoja anamiliki vitalu vikubwa sana vya uwindaji. Ni suala la faida na mamlaka!
27. **Maoni (Mbunge, Longido):** Jimbo lake lina vitalu vingi vya uwindaji, hivyo amefurahishwa sana na mjadala wa leo. Maamuzi ya mwisho yatakayotolewa ni vema yazingatie matakwa ya jamii.
28. **Maoni:** Hii siku moja fupi yaweza kuleta matatizo zaidi kama hatutaweza kusikilizana na kuelewana. Nani atalaumiwa kwa kutokuelewana? Kwanini raia hulaumiwa mara nyingi kwa kuvunja sheria na wakati sheria zenyewe haziko wazi?
29. **Maoni**: Wawindaji hawapigi hodi; wanaonyesha tu cheti kutoka wizarani. Hii ni dharau kwa jamii. Huu ndio mkutano wa kwanza tumepata kuwa na Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori na manaibu wakurugenzi. Tafadhali fanyeni ziara katika kila wilaya ili kuja kujadili masuala haya katika ngazi ya chini.
30. **Maoni (Mbunge wa Longido):** Kila kijiji ni tofauti. Ziara za Idara ya Wanyamapori ni muhimu mno. Kabla ya uanzishwaji wa Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) vijiji vingine hawakuarifiwa na wala hawakupata habari ya kuwahamasisha.
31. **Maoni:** Pamoja na kuwa serikali ina malengo mazuri kwa kurudisha majukumu ya usimamizi wa wanyamapori baadhi ya makampuni na asasi zisizo za kiserikali (NGOs) wana nia mbaya ambayo inaishia kuwaumiza wanajamii.
32. **Maoni (Longido, Halmashauri ya Wilaya):** Kama mababu zetu walijua jinsi ya kusimamia wanyama, wanyama wote tulio nao leo hapa wasingekuwepo. Wengi kule Longido hawakupewa nafasi ya kuchangia katika mdahalo juu ya uanzishwaji wa Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA).
33. **Maoni (kutoka Ngorongoro):** Inapendeza kuona wadau mbalimbali tupo pamoja. Tunahitaji ufafanuzi juu ya hali ya Mapoti Tengefu (GCA). Tunaendeleaje huku tukifuata sheria?
34. **Maoni (kutoka Asasi isiyo ya kiserikali):** Hatuelewi nani mwenye mamalaka ya kuitisha mkutano wa Bodi ya Ushauri ya Wilaya.

35. **Maoni (kutoka Asasi isiyo ya kiserikali):** Je kampuni moja yaweza kuwa na "hatimiliki" (milki) ya kutumia raslimali wanyamapori katika vijiji kadhaa?
36. **Maoni:** Wawekezaji walipewa vibali na sasa wana majengo ya kudumu katika Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) pamoja na kuwa wana miaka mitatu tu ya mkataba. Je, wawekezaji hawa wanaweza kumiliki ardhi? Sehemu kubwa ya wilaya ni maeneo ya hifadhi, hivyo tunategemea zaidi utalii kwa maisha yetu.
37. **Maoni (Mkuu wa wilaya Longido):** Sheria nyingi zinapingana. Halmashauri ya Wilaya ina mamlaka juu ya halmashauri za vijiji, na hivyo hakuhitajiki tena kuwe na sheria kama ilivyopendekezwa na mwanasheria (Maoni Namba 13).
38. **Maoni (Mkuu wa Wilaya, Ngorongoro):** Maamuzi yote na dharura ilitakiwa kuwa vimefikiriwa kwa makini.
    TNRF ni nani na hata wana uwezo wa kuwaalika viongozi wa serikalikwenye mkutano? Inawezekanaje mtu wa nje aingie nchini na aanze kuwekeza bila hata kufuata taratibu halali za uhamiaji. Tunahitaji mwakilishi kutoka ofisi ya Waziri Mkuu kwa masula ya tawala za mikoa na serikali za mitaa (TAMISEMI).
39. **Maoni (Mbunge, Longido):** Sheria hazipingani. Kuna matatizo zaidi mawili: Wawekezaji na umbali mrefu wa kutembea toka vijijini hadi ofisi za wilaya. Mbunge huyu ni mjumbe wa Kamati ya Bunge inayoshughulikia Maliasili na Mazingira, na baada leo atapeleka mjadala katika kamati yake.
40. **Maoni (Afisa Wanyamapori, Wilaya ya Ngorongoro):** Maliasili ni vizuri zikawa na faida kwa jamii. Ushirikishwaji jamii ni muhimu katika kufanya maamuzi ya mwisho.
41. **Maoni (kutoka Asasi isiyo ya kiserikali):** Dola 25,000 (USD) kama ada ya uhifadhi haiwafikii wananchi. Fedha hizo zinatumikaje? Tumeshaona kuwa watu wanapoona hawafaidi kutoka katika maliasili, wanaanza kuvunja sheria.
42. **Maoni** (Naibu Mkurugenzi, Maendeleo ya Wanyamapori): Mara mapato yakishakusanywa hupelekwa hazina. Ndipo Idara ya Wanyamapori huomba fungu la fedha ili kurudishwa katika halmashauri husika na Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA). Kiwango cha mapato kilichokusanywa na kinachotakiwa kurudishwa bado havijaamuliwa
43. **Swali:** Je tunaweza kuona masula ya mifugo yakiakisiwa katika Sera ya Wanyamapori, Sheria na Kanuni?
44. **Maoni (kutoka Asasi zisizo za kiraia):** Sera ya Wanyamapori (1998) haigusii migogoro kati ya wanyamapori mashamba na mifugo.
45. **Swali:** Watu walitaka kujua juu ya tathmini ya Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA). Kama tarifa ni tayari nini matokeo yake?
    **Jibu:** Taarifa tayari na sasa inawekwa katika lugha rahisi kwa ajili ya kusambazwa kwa umma.
46. **Maoni (kutoka kampuni ya utalii):** Kuna masomo tumejifunza kutoka programu za usimamizi wa kijamii wa maliasili katika nchi zingine kama vile CAMPFIRE huko Zimbabwe. Tunawezaje kwa pamoja kujifunza kutoka katika uzoefu huo?
47. **Swali:** Nini kifanyike katika elimu kwa Jamii juu ya mafao ya maeneo ya Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA)? Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) ni dhana mpya na vijiji vingi walipokea bila kujua masuala ya usimamizi na thamani yake.
48. **Maoni (kutoka kampuni ya utalii):** Tutumie mapato zaidi kutoka kutoka Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) kuelimisha jamii juu ya thamani ya uhifadhi wa kijamii wa wanyamapori. Hata sisi leo hapa ambao ni viongozi katika usimamizi wa kijamii wa wanyamapori bado hatuna habari za msingi za masuala yanayotukabili.

49. **Maoni (Afisa wanyamapori Ngorongoro):** Pamoja na changamoto nyingi bado kuna visa vya mafanikio katika mfumo huu wa hifadhi za kijamii kwa vile kila kisa ni tofauti na kingine. Tufanye bidii ili kubadilishana visa vya mafanikio
50. **Maoni (Mbunge wa Longido):** Waelimishaji kutoka Asasi zisizo za kiserikali mara nyingi huja na habari mchanganyiko na huhusisha tu viongozi waandamizi wa serikali.
51. **Maoni (Mkuu wa Wilaya, Longido):** Tunahitaji tathmini ya Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) yaliyofanyiwa majaribio.
52. **Maoni (Naibu Mkurugenzi, Maendeleo ya Wanyamapori):** Tathmini ya Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) imefanyika, ila iko katika lugha ya Kiingereza na sasa inatafsiriwa kwa Kiswahili.

## 2.7 Mada juu ya Kanuni za Uhifadhi wa Wanyamapori, Matumizi yasiyo ya Uvunaji (2007), na Kaimu Mkurugenzi, Matumizi ya Wanyamapori, Mr. Mohammed Madehele

1. Hapo awali matumizi yote yasiyo ya uvunaji yalikuwa yakifanyika katika Hifadhi za Taifa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. Kutokana na ongezeko la watalii na juhudi za kitaifa kukuza uchumi wa wananchi makampuni mengi yameanza kuwekeza katika maeneo ya wazi nje ya Hifadhi za Taifa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.
2. Serikali ilikosa mfumo thabiti wa ufuatiliaji, uwekezaji na kukusanya mapato na uwekezaji haukuwa na utaratibu maalumu na hivyo maduhuli yakapotea.
3. Watanzania wachache walifaidika kutoka katika mfumo huu uliokosa viunzi vya asasi. Walikusanya maduhuli baada ya kusaini mkataba na wawekezaji.
4. Kutokana na kukosekana kwa miongozo inayoweka mfumo wa ada kwa wawekezaji, kila kijiji kiliweka mfumo wake wa ada. Baadhi ya vijiji vikajikuta vinalippwa fedha ndogo chini ya wastani. Mfumo huu wa hadhi uliwafaidisha Watanzania wachache.
5. Serikali baada ya kugundua mapungufu hayo iliamua kuingilia kati kwa kuanzisha kanuni kusimamia matumizi ya wanyamapori yasiyo ya uvunaji ili kutetea na kulinda masilahi ya wengi.
6. Malengo ya Kanuni za the Matumizi yasiyo ya Uvunaji wa Wanyamapori:
    a. Kutoa miongozo kwa uwekezaji katika matumizi yasiyo ya uvunaji ya wanyamapori na kutatua migogoro inayojitokeza kutokana na matumizi ya raslimali wanyamapori;
    b. Kusaidia katika usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za matumizi ya wanyamapori yasiyo ya uvunaji;
    c. Kupanga mfumo wa ada na kufuatilia ukusanyaji wa mapato ya serikali kutokana shughuli za matumizi yasiyo ya uvunaji wa wanyamapori;
7. Kanuni zinaweka utaratibu utakaofuatwa kabla ya uwekezaji, ambayo huhusisha:
    a. Kumiliki kampuni iliyosajiliwa na mamlaka zinazotambuliwa;
    b. Kuwa na ofisi inayojulikana;
    c. Kuwa na cheti kutoka mamlaka sahihi ya kutathmini athari za kimazingira;
    d. Kuongoza wawekezaji ambao husaini mikataba na mamlaka husika (Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori na wadau wengine) ili kukuza na kuendeleza biashara juu ya matumizi yasiyo ya uvunaji wa raslimali wanyamapori;
    e. Kulipa ada zote kama zilivyoelekezwa na Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori;
    f. Kukubaliana na masharti mbalimbali ya uwekezaji kama yanavyotolewa na Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori;
8. Kufuatilia matumizi yasiyo ya uvunaji wa raslimali wanyamapori:

a. Mkataba ndio waraka muhimu kusaidia ufuatiliaji matumizi yasiyo ya uvunaji wa raslimali wanyamapori.
b. Mkataba lazima uainishe masuala yafuatayo:
    i. Shughuli zinazotakiwa
    ii. Kanda za matumizi na mipaka yake
    iii. Mchakato wa ujenzi wa makambi na hoteli na udhibiti wa ubora kulingana na nguvu za soko
    iv. Masuala ya kuanisha baada ya kumaliza ujenzi na wakati wa uendeshaji halisi wa biashara
    v. Njia za kulipa malipo mbalimbali, muda wa malipo na walipwaji
    vi. Makubaliano mengine kati ya mwekezaji na mmiliki wa raslimali
    vii. Tarehe za mwanzo na mwisho wa mkataba
    viii. Njia za utatuzi wa migogoro

9. Kutatua migogoro juu ya matumizi ya raslimali wanyamapori:
    a. Kanuni zitasaidia kutatua migogoro juu ya matumizi ya raslimali wanyamapori kwa sababau migogoro mingi inatokana na kukosa usimamizi madhubuti katika shughuli za uwekezaji katika vitalu vya uwindaji, Maeneo ya Wazi na Ardhi ya Kijiji.
    b. Kanuni zinampa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori mamlaka ya kufuatilia maendeleo na mchakato wa matumizi yasiyo ya ulaji nje ya maeneo yaliyohifadhiwa kama vile Hifadhi za Taifa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCA).
    c. Kila mwekezaji ni lazima awasiliane na Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori kwamba kampuni inasaini mkataba na pia apewe kibali kinachoruhusu kupata leseni ili kuendelea na ulipaji wa TALA.
10. Mfumo wa Ada
    a. Kanuni imeweka mfumo wa ada kwa shughuli mbalimbali za matumizi yasiyo ya uvunaji. Hiyo ni pamoja na:
        i. Ada za viingilio kwa wageni na magari
        ii. Ada za upigaji filamu
        iii. Ada za kupiga makambi
        iv. Ada za mitumbwi na chelezo
        v. Ada ya safari za usiku
        vi. Ada ya safari za miguu
        vii. Ada za viwanja na Maputo ya moto
        viii. Ada ya uhifadhi
        ix. Ada ya uvuvi burdani
        x. Ada ya haki ya kutumia
        xi. Ada ya kuongoza wageni
        xii. Ada ya kuongoza wageni katika maeneo yaliyohifadhiwa

## 2.8 Mjadala kimakundi

Baada ya mjadala wa wote Mkurugenzi aliwaalika wajumbe kujadili mambo yawahusuyo kwa undani katika vikundi vidogo kulingana na mada katika matumizi ya wanyamapori. Kila kundi lilitakiwa kuja na mapendekezo ya kuboresha kwa mada waliyopewa: Mada hizo ni:

- Mgawanyo wa mapato
- Mfumo wa kupanga ada

- Usimamizi wa vitalu vya uwindaji
- Utatuzi wa migogoro

Mapendekezo yote yanayofuata hapo chini yalitolewa kutoka mabango kitita.

### 2.8.1 Mawasilisho juu ya mgawanyo wa mapato

***A. Mapendekezo:***

i. Mapato ni budi yagawanywe kwa haki ili kuzuia migogoro.
ii. 35% serikali kuu
iii. 65% Serikali za mtaa hupata zaidi kwa vile wananchi wako karibu na migogoro ya wanyamapori
iv. Serikali za mtaa kupata asilimia 65 ya mapato kunatokana na sababu zifuatazo:
    b. Jamii huathirika zaidi na wanyama
    c. Wananchi wanaoishi pamoja na wanyamapori hawawezi kufanya shughuli zingine za uzalishaji mali kirahisi kama vile ufugaji na kilimo.
v. Wakati asilimia 65 ikifika katika Halmashauri ya wilaya, 60% inatakiwa iende kwa jamii na asilimia 40 iende katka matumizi ya Halmashauri ya wilaya.

***B. Mwitikio wa mjadala:***

**Angalizo:** Baadhi ya washiriki waliona kuwa mfumo wa sasa wa ada haufai na mgawanyo wa mapato hauko wazi. Ada ni lazima zigawanywe kwa haki miongoni mwa vijiji vyenye Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) ili kuepuka migogoro.
**Mkuu wa Wilaya, Ngorongoro:** Alipendekeza 25% kwenda Halmashauri ya wilaya na 40% kwenda serikali za vijiji.

### 2.8.2 Mawasilisho juu ya mfumo wa ada

**Angalizo la Sekretariet ya TNRF:** Mijadala haikuwezeshwa vizuri na hivyo ilisababisha majadiliano katika vikundi kutokuongozwa na kuwezeshwa vizuri, hivyo kutokuleta matokeo yaliyotarajiwa hasa. Hivyo itahitaji maboresho zaidi. Sehemu yote ya mfumo wa ada imeachwa.

***A. Mapendekezo:***

i. Kundi liliunga mkono mapendekezo ya mifumo ya bei kwa maeneo yaliyohifadhiwa na upigaji wa makambi.
ii. Ada katika Vitalu vya Uwindaji
    - Raia umri wa miaka 18 na zaidi…5000/-
    - Raia umri 5-17…3000/-
    - Raia umri 5…BURE
    - Wageni umri 18 na zadi…$50
    - Wageni umri 5-17…$30
iii. Mapori Tengefu
    - Raia umri 18 na zaidi…2000/-
    - Raia umri 5-17…1000/-
    - Raia umri 5…BURE
iv. Upigaji Piga za kibiashara
    - Raia umri 18 na zaidi… 50,000/-
    - Raia umri 5-17… 40,000/-

- Raia umri 5… BURE
- Wageni umri 18 na zaidi…$200
- Wageni umri 5-17… $150

v. Katika maeneo ambayo hayana Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) au Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA), ukusanyaji wa ada utafanywa na halmashauri za wilaya kwa ushirikiano na serikali kuu. Mahali ambapo Jumuia za kijamiii zipo zishirikishwe katika ukusanyajiwa ada zilizotajwa hapo juu.

### 2.8.3 Mawasilisho juu ya usimamizi wa vitalu vya uwindaji

### 2.8.4 *A. Mapendekezo:*

i. Maombi ya vitalu vya uwindaji katika Mapori ya Akiba yapelekwe moja kwa moja kwa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori

ii. Maombi ya vitalu katika Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) yapitie kwenye Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA). Baada ya kujadiliwa maombi yatapelekwa kwenye Bodi ya Ushauri ya Wilaya na baadae kwa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori kwa idhini ya mwisho. Ni wajibu wa Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) kufuatilia kwa karibu vitalu katika Maeneo ya Hifadhi za Wanyamaopri za Jumuia (WMA).

***B. Mwitikio wa mjadala:***

Kuna baadhi ya wajumbe walikuwa na mtazamo kwamba wawindaji walikuwa wanajiona kama nusu-miungu, hivyo ni vyema Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) ijitahidi kutimiza wajibu wao na kuyafuatilia makampuni ya wawindaji na wawajibike kwa mikutano ya hadhara vijijini.

### 2.8.5 Mawasilisho juu ya Utatuzi wa Migogoro ya matumizi ya Raslimali

***A. Mapendekezo:***

i. Njia za Utatuzi wa Migogoro

- Kila eneo liwe na mpango wa matumizi bora ya ardhi. Mpango huu ni budi uheshimiwe na kufuatwa na wadau wote.
- Kanuni, sheria na mchakato ni budi vifuatwe na makundi yote.
- Kama mgogoro ukijitokeza, utatuzi uanze na majadiliano miongoni mwa wahusika tu

ii. Kama majadiliano ya awali yameshindikana, wahusika waende kwenye bodi ya ushauri ya wilaya katika maeneo ya hifadhi ya vijiji kwa ushauri zaidi.

- Na kama bodi ya ushauri ya wilaya ikishindwa, basi, wahusika wamchague msuluhishi ambaye anakubalika pande zote.
- Na kama msuluhishi akishindwa, wahusika wapeleke shauri lao mahakamani. Pia, mikataba ni budi ipitiwe mara kwa mara
- Adhabu kali itolewe kwa mwekezaji anayevunja sheria.

| Aina ya Mgogoro | Utatuzi |
|---|---|
| 1. Matumizi ya ardhi zaidi ya moja (i.e. uwindaji, upiga picha, uchungaji, uwindaji wa kiraia) | Hamasa ya kanuni zinazohusika na masuala. |
| | Masharti lazima yaelezwe kwamba wawindaji lazima wapitie serikali za vijiji wanaomiliki maeneo hayo kupata ukubali. |

| | |
|---|---|
| **Hakuna utaratibu na maelewano ni kidogo kwa pande zote mbili.** | Vibali na miliki za uwindaji zisitolewe bila kushirikisha wananchi katika mchakato wa kufanya maamuzi. |
| 2. Makampuni ya uwindaji kuingiliana katika vitalu au kugombana juu ya mipaka ya vitalu i.e. zaidi ya kampuni moja kuwinda katika kitalu kimoja. | Makampuni ya uwindaji vyema yaheshimu mamalaka ya vijiji. |
| | Mchakato ni budi ufuate mipaka iliyowekwa ya kisheria. |

# 3 MAKAMPUNI YA KITALII NA WAWEKEZAJI

## Siku ya 2 Mkutano uliendeshwa kwa lugha ya Kiingereza

**Angalizo la Sekretariet ya TNRF:** Kwa ujumla siku ya pili uliendeshwa vizuri zaidi. Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori aliweza kuhudhuria. Bahati mbaya muhtasari wa kumbukumbu za siku ya kwanza haukuandaliwa na hivyo kumaanisha kuwa mwendelezo wa mikutano katika siku hizo mbili haukuwepo. Kilichosaidia ni kwamba mawazo ya mwendelezo yalitolewa na baadhi ya wajumbe ambao walichagua kujihudhurisha katika mikutano yote miwili na walisaidia sana kwa mawazo yao. Kwa ujumla mkutano ulifanyika katika hali ya kujengana, ukiruhusu midahalo na majadiliano. Ingawa baadhi ya matokeo ya mkutano kwa siku ya pili yalikuwa hayana upinzani, lakini bado mwishoni hakukuwa na suluhisho au makubaliano ya nini kifanyike kuhusu matumizi ya wanyamapori yasiyo ya uvunaji kufuatia Kanuni Mpya, Tangazo la Serikali na. 196 (2007). Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori aliahidi kuyajadili mapendezo ya mkutano pamoja na Waziri katika kurekebisha na kuzifanya kanuni ziweze kutumika. Kwa misingi hiyo wadau wengi katika utalii wangependa kufahamu lini, vipi na wapi ada katika Kanuni Mpya.

### 3.1 Utambulisho kimakundi

**Washiriki**

- Makampuni ya utalii wa picha
- Makampuni ya uwindaji wa kitalii
- Wawekezaji
- Vyama vya hiari
- Asasi zisizo za kiserikali (NGOs)
- Halmashauri
- Wakuu wa Wilaya
- Idara ya Wanyamapori

### 3.2 Sala

Sala zilitolewa kwa ombi la Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori wakati wa mkutano unapoanza.

### 3.3 Utambulisho na Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori

Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori alitambulisha ajenda na akataja Kanuni za Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori ya 1974 (Rekebisho la 2002) ambalo litajadiliwa ikijumuisha:

- Uhifadhi wa Wanyamapori (Uwindaji wa Wanyama) Kanuni: Tangazo la Serikali Na. 272 (1974)
- Uhifadhi wa Wanyamapori (Ukamataji Wanyama Hai) Kanuni: Tangazo la Serikali na. 274 (1974)
- Uhifadhi wa Wanyamapori (Uwindaji wa Kitalii) Kanuni: Tangazo la Serikali na. 306 (2002)

- Uhifadhi wa Wanyamapori (Uwindaji wa Wanyama) Kanuni: Tangazo la Serikali na. 196 (2007)

Kama ilivyokuwa siku ya kwanza Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori aliwakaribisha vizuri wajumbe na kuwaomba wachangie ajenda. Alisisitiza uwazi na kwamba ofisi yake iko wazi kwa kwa kila oni na hitaji na alipenda kuanza sura mpya katika suala la uhifadhi wa wanyamapori.

## 3.4 Mada juu ya "Kanuni za matumizi mbalimbali ya wanyamapori" na Kaimu Mkurugenzi, Matumizi ya Wanyamaporim, Bw. Mohammed Madehele

a. Makundi ya Kiuhifadhi:

<table>
<tr><td>i. Hifadhi za Taifa</td><td>Sheria Cap. 282 pitio la 2002</td></tr>
<tr><td>ii. Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro</td><td>Sheria Cap. 284 pitio la 2002</td></tr>
<tr><td>iii. Mapori ya akiba</td><td rowspan="3">Sheria Act. 283 pitio la 2002 (WCA),</td></tr>
<tr><td>iv. Mapori tengefu</td></tr>
<tr><td>v. Bustani za wanyama, mashamba ya wanyama, ranchi</td></tr>
</table>

b. Maeneo mengine ya jumla yasiyo na hadhi ya kiuhifadhi:
   i. Maeneo ya hifadhi ya Jamii (katika ardhi za vijiji)
   ii. Maeneo ya Wazi (hayana hadhi ya kiuhifadhi)

c. Kanuni zinazosimamia matumizi ya wanyamapori katika Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA), Mapori Tengefu na Maeneo ya wazi:
   i. Uhifadhi wa Wanyamapori (Kuhusiana na Nyara) Kanuni: Tangazo la Serikali Na. 268 (1974) inahusu vyeti, masharti ya kupeleka nyara nje ya nchi, na ufuatiliaji.
   ii. Uhifadhi wa Wanyamapori (Uvunaji) Kanuni: Tangazo la Serikali na. 272 (1974) huhusu masharti ya leseni, ada na uhalali.
   iii. Uhifadhi wa Wanyamapori (Ukamataji Wanyama Hai) Kanuni: Tangazo la Serikali Na. 274 (1974) huhusu masharti ya utoaji na mfumo wa vibali, wajibu wa wakamataji, maeneo ya kutunzia, maslahi na usalama wa wanyama na pia utoaji taarifa.
   iv. Uhifadhi wa Wanyamapori (Uwindaji wa Kitalii) Kanuni: Tangazo la Serikali Na. 306 (2002) huhusu ugawaji wa vitalu, masharti, ada za wanyama, muda wa vitalu, vigezo vya tathmini na ufutaji wa vitalu katika Mapori ya Akiba, Mapori Tengefu and Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA).
   v. Uhifadhi wa Wanyamapori (Matumizi yasiyo ya Uvunaji wa Wanyamapori) Kanuni: Tangazo la Serikali Na. 196 (2007): Hii kanuni ndio kiini cha mada hii. Itarekebisha Matumizi yasiyo ya Uvunaji wa Wanyamapori nje ya maeneo ya Hifadhi za Taifa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA). Maeneo haya hujumuisha Mapori ya Akiba (GR), Mapori Tengefu (GCA), Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) and Maeneo ya Wazi. Malengo muhimu ni:
      1. Kutoa miongozo ya uwekezaji katika maeneo;
      2. Kutoa utaratibu wa kiutendaji katika maeneo husika;

3. Hutoa viwango vya ada kwa matumizi mbalimbali ya shughuli zisizo za uvunaji zinazoendeshwa katika maeneo;
4. Kutatua migogoro inayojitokeza miongoni mwa wadau.

Kanuni hizi pia hutoa viwango vya ada zifuatazo:

- Magari na viingilio binafsi
- Upigaji picha kibiashara
- Ada za kambi
- Ada za Mashua, Mitumbwi na chelezo au boya.
- Utalii wa picha - Usiku
- Ada za utuaji
- Gharama za viwanja
- Ada za matembezi
- Uvuvi wa burdani
- Ada za Maputo ya joto
- Ada za uhifadhi na haki ya kutumia
- Ada za wanataluma waongoza wageni
- Ada za kawaida za kuongoza wageni

Kuhusiana na migogoro ya matumizi ya wanyamapori miongoni mwa wadau itaanza kutumika rasmi mnamo Julai mosi 2008.

vi. Mswada wa Uhifadhi wa Wanyamapori uko katika hatua za mwisho za uandaaji ili kuuwasilisha Bungeni.

Naibu Mkurugenzi, Matumizi ya Wanyamapori alisisitiza kuwa michango toka kwa wadau wote katika rasmu hii ni ya muhimu kwa ufaaji wa Kanuni kwa vile wadau ndio wanaoathirika na utekelezwaji wa kanuni husika. Washiriki walitakiwa na kuhimizwa kutoa mawazo na mapendekezo yao.

## 3.5 Michango ya wote

***Michango ya wajumbe juu ya mada zote ilioroodheshwa pamoja na wawasilishaji wa mada na mwishowe ikajibiwa kwa kufuata moja baada ya jingine. Maelezo yafuatayo hapa chini yameandaliwa na Sekretariet ya TNRF ili kuyalinganisha majibu yaliyotolewa na maswali yaliyoulizwa.***

1. **Swali (Kampuni ya utalii wa picha):** Ni nini tofauti kati ya kanuni za matumizi ya wanyamapori ya matumizi yasiyo ya uvunaji na miongozo?
   **Jibu (Mkurugenzi):** Kanuni zitaanza kutumika Julai Mosi 2008. Miongozo ni tofauti na imeandaliwa katika hali rahisi kuwasaidia watumiaji kuelewa kanuni. Kanuni pia zaweza kutafsiriwa toka lugha Kiingereza na kwenda katika lugha ya Kiswahili. (Kwa sasa miongozo haijatolewa).
2. **Swali:** Mshiriki alitaka ufafanuzi wa mada ya mwanasheria. Kwanini Mapori Tengefu yamejumuishwa?
   **Jibu (Mkurugenzi):** Makundi hayo yamejumuishwa kimakosa. Mapori Tengefu (GCA) hayakutakiwa kuchanganywa hapo. Zingatieni kuwa Mamlaka ya Ngorongoro ni eneo pekee chini ya sheria,

1959. Wanavijiji katika eneo la Ngorongoro wana haki ya kutumia eneo lakini sio hati miliki, hii inamilikiwa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kulingana na sheria ya Mamlaka na Katiba.

3. **Maoni (Katibu Mtendaji, Chama cha makampuni ya utalii, TATO):** Kuna mgongano katika sheria, tunahitajika kufanya kitu.

   **Jibu (Mwanasheria, Kamisheni ya Ardhi):** Baadhi ya vijiji viko katika Mapori Tengefu (GCA). Rejea Kifungu Na. 6 Sheria ya Ardhi (1999). Maeneo mengine yametengwa kama Ardhi iliyohifadhiwa, Ardhi ya Jumla na Ardhi ya Vijiji. Vjiji katika maeneo haya vina vyeti vya kuwawezesha wao kusimamia ardhi kwa niaba ya wanavijiji. Suala hili lina utata na linahitalijadiliwe kadara ya Wanyamapori na Wizara ya Ardhi. Kinachohitajika ni kutofautisha kati ya haki za ardhi na haki za matumizi ya wanyamapori.

   **Jibu (Mkurugenzi):** Hati za kumilki ardhi katika Mapori Tengefu zilitolewa kimakosa. Idara kwa sasa inafanya mapitio ya Mapori Tengefu yote kuona vijiji vyenye vyeti ili kuruhusu ufutaji wa hadhi ya Mapori Tengefu katika vijiji husika na kubadilishwa kuwa maeneo ya Hifadhi ya Vijiji. Ni kosa kuwa na hati miliki katika maeneo ya Mapori Tengefu. Rais amefahamishwa ili asaidie kutatua tatizo hili.

   **Angalizo la Sekretariet ya TNRF:** Hati miliki hazijaelezewa wala hazihusuki katika Mapori Tengefu kwa sababu hati milki na vyeti vya ardhi ya kijiji vilikuja kabla ya uanzishwaji wa Mapori Tengefu.

4. **Swali (Kampuni ya utalii wa picha - Natron):** Je itawezekana kuwa na ada tofauti kwa maeneo yaliyo muhimu na wanyama wengi na yale yaliyo na wachache?

   **Jibu (Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori):** Ni mapema mno kulisemea hili kwa sasa. Ni makampuni mangapi kwa kweli hulipa ada hii?

   **Angalizo la Sekretariet ya TNRF:** Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori aliuliza swali hili katika muktadha wa tatizo la kwamba baadhi ya makampuni yanaweza kuwa hayalipi ada zao.

5. **Maoni (Kampuni ya uwindaji):** Makampuni ya wageni huleta watalii wengi. Lazima tukumbuke hali ya soko. Kama kuna ada nyingi, ni namna gani tunaweza kurekebisha mfumo? Mfumo utakuwa mgumu kuurekebisha na kuusimamia. Kama ada ziko juu mno, tutatupwa nje ya soko na nchi majirani ambao wana mfumo rahisi.

   **Jibu (Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori):** Sheria na Kanuni ni za muhimu kwa kulinda utaratibu.

6. **Swali (Kampuni ya utalii wa picha):** Sokwe Asilia wamekuwepo Loliondo kwa miaka na mwanzoni ilikuwa ni Hifadhi ya Taifa ya Serengeti iliyoiomba kampuni kuanzisha uwekezaji katika maeneo ya jamii ili kukuza uchumi wa jamii. Hata hivyo, hivi karibuni kampuni imeanza kukatazwa kufanya kazi zake nje ya hifadhi. Kwanini? Tunawezaje kutatua tatizo la kampuni mbili (moja ya picha, nyingine ya uwindaji) wakiwa na mikataba miwili tofauti – wapiga picha kutoka katika kijiji na wawindaji kutoka Idara ya Wanyamapori – kwa kufanya kazi kwenye eneo moja la ardhi?

   **Jibu (Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori):** Suala hili ni budi lifanywe kiofisi. Majadiliano ya leo yatatoa mapendekezo muhimu kwa Idara ya Wanyamapori ili kusaidia kutatua suala hili. Mkutano wa kwanza ulifanyika Loliondo kuanzisha majadiliano hayo kwa undani zaidi nab ado yanaendelea.

7. **Swali (Mwekezaji):** Ni mikataba ipi wawekezaji watatakiwa kusaini na wanakijiji au katika maeneo ya Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) na Jumuia za kijamii zilizoidhinishwa (AA)? Kampuni yetu imepokea barua kutoka katika kijiji kuwa kampuni isisaini mkataba wowote na Jumuia ya jijamii iliyoidhinishwa (AA). Rejea Kifungu cha 22 cha Kanuni ya Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA), Sehemu "J" ambayo inatamka kwamba Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) iombe idhini ya kutoka mkutano wa hadhara wa kijiji kwa ajili ya uwekezaji katika ardhi yao. Tufanye nini kama mwekezaji alikuwa anafanya kazi katika eneo husika kabla ya uwepo wa Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA)?

**Jibu (Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori):** Sheria iko wazi katika suala hilo na ndio tunachotaka kufafanua kwa leo.

**Jibu (Naibu Mkurugenzi, Maendeleo ya Wanyamapori):** Kuna masuala mawili hapa katika muktadha huu: upataji wa ardhi na matumizi ya wanyamapori. Mwekezaji lazima asaini mkataba na Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) ili kutumia wanyamapori, lakini pia asaini mkataba mwingine na serikali ya kijiji kwa haki maalumu ya kutumia ardhi.

**Jibu (Mwanasheria, kutoka Wizara ya Ardhi):** Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) huwajibika kwa serikali ya kijiji. Wawekezaji wanavichanganya vijiji. Sheria ziko wazi. Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) ni lazima kupitisha idhini ya mwekezaji kupitia mkutano wa hadhara wa kijiji na Halmashauri ya Wilaya. Kama mwekezaji alikuwa akifanya kazi katika eneo kabla ya kuwepo kwa Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA), mwekezaji bado atatakiwa kupitia the Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) kama taratibu.

**Jibu (Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori):** Mazungumzo ya leo yatakuwa ya ujumla. Tutapata fursa wakati mwingine kuongelea kila kisa kwa undani wake.

8. **Maoni:** Nafasi ya serikali ni kuongeza utajiri wa raslimali na kuhimiza biashara katika sekta ya utalii. Hata hivyo Kanuni Mpya haziwawezeshi wawekezaji kufanya biashara kwa urahisi, mada ya Naibu Mkurugenzi juu ya hizo kanuni una kasoro kwa watumiaji. Mfumo wa ada uko kinyume na lengo la kitaifa la kukuza idadi ya watalii. Katika utafiti uliofanywa na Idara ya Mapato nchini wakishirikiana na TANAPA na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro imegundua kwamba viwango vya tozo kwa sasa wageni waingiao Serengeti ni dola 50 (USD). Kenya, viingilio vya wageni kitaifa ni dola 40 (USD) na Uganda ada ni dola 25 (USD). Ada zilizopendekezwa kwa Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) ziko juu zaidi ya hizo wakati uwezo wa kuvuta wageni katika maeneo haya utakuwa ni kidogo sana. Matokeo yake ni kwamba Tanzania haitaweza kushindana katika masoko ya kikanda. Ni sekta binafsi ndio huleta fedha serikalini na hivyo sekta binafsi iruhusiwe kushindana. Kanuni kifungu 11.1 kinahusu kuitaarifu serikali wakati hisa za kibiashara zinahama. Kanuni hii si sahihi kwa vile kama hisa za kampuni zimesajiliwa na kuuzwa katika soko la hisa kutaarifiwa kutakuwa ni vigumu.

   **Jibu (Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori):** Huduma za Wanyamapori Kenya (KWS) nao sasa wanapandisha ada zao ili zilingane na za kwetu. Ni vigumu kulinganisha ubora wa hifadhi na vivutio vilivyo nje ya hifadhi, kwa sababu kila eneo lina upekee wake. Lakini ni kweli pia wawekezaji wanachangia sana katika suala zima la uhifadhi.

9. **Maoni (Kampuni ya utalii na hoteli):** huchukua karibu mwaka mmoja kujipanga sawa na ongezeko la ada kwa sababu ya kuchelewa katika mikondo ya soko. Mawakala wa nje wanaona Tanzania itapoteza soko lake kwa sababu ya kupanda kwa bei. Wageni wengi wa kampuni ya Serengeti Select Safaris wanapenda kutumia muda wao vijijini wakijifunza na kuchangia katika maendeleo ya shule na kanisa. Kwa ujumla vikundi hivi hawawezi kulipia gharama hizo za juu. Mara tu soko la utalii la Tanzania litakapotamkwa kama ni soko la gharama mno, itakuwa vigumu kurudisha tena hadhi ya soko la unafuu.

   **Jibu (Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori):** Hatupendi tuwe na sura ya kupokea watalii wachache wanaolipa zaidi kama Amboseli, hata hivyo ada zenye haki ndio hitaji la msingi.

10. **Maoni (Katibu Mtendaji, TATO):** Katika mwaka 2005 Waziri wa Maliasili na Utalii alisema kuwa hakutakuwa na ongezeko la ada hadi hapo tafiti katika masoko itakapokuwa imefanyika. Kinyume chake ada zimeendelea kupanda, sasa TATO itatoa utafiti wake. Kuna mambo mengi yanayokinzana na hivyo tutahitaji mazungumzo.

    **Jibu (Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori):** Tuna dhana mpya katika utendaji kwa sasa kwa serikali ya Tanzania na hivi karibuni tunategemea kuona mabadiliko makubwa.

11. **Maoni:** Soko ni tete, linahitaji tafiti ili kulielewa. Lazima tulenge zao husika.

**Jibu (Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori):** Kanuni zimebuniwa kwa wakati na zitasaidia. ***Swali toka kwa Mkurugenzi***: Je kuna mtu hapa anayeelewa ni kiasi gani waendesha utalii wanailipa serikali kodi?

**Angalizo la Sekretariet ya TNRF:** Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori alikuwa akirejea katika uwezekano kuwa inawezekana ikawa si makampuni yote hulipa ada zote zinazotakiwa hususa ni dola 25,000 (USD) kama ada ya uhifadhi.

**Jibu (Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori):** Kuendesha gari usiku ni zao jipya la kitalii ambalo ndio linazinduliwa na inaweza kuongeza utafutaji wa soko la Kitanzania. Uendeshaji gari usiku ambao waweza kuwa umefanyika huko nyuma haukuwa halali.

## 3.6 Mjadala kimakundi

Washiriki waligawanywa katika makundi manne ili wajadili katika makundi madogo na kutoa mapendekezo katika maeneo malumu. Maeneo hayo yalikuwa:

- Mfumo wa ada na taratibu za malipo
- Ni vipi watumiaji wote wa raslimali wanaweza na kufanya kazi mahali pamoja?
- Uchaguzi wa kugawana mapato na mafao
- Nafasi ya watumia raslimali katika ulinzi wa maliasili

Makundi yalichaguliwa kwa mchanganyiko na walipewa maswali mawili kujadili kabla ya kutoa mrejesho. Utendaji wa kila kundi ulitofautiana sana kwa kila kundi kutegemeana na uwezo wa mwenyekiti wa kikundi. Katika makundi mengine wazungumzaji wa asili ya Kiingereza walitawala mazungumzo wakati katika makundi mengine masuala ya visa mahsusi na pengine migogoro ndiyo iliyotawala mjadala.

### 3.6.1 Mawasilisho1: Mfumo wa Ada na Utaratibu wa Malipo

**A. Mapendekezo:**

i. Ilipendekezwa kuwa mfumo wa ada uliopendekezwa usitekelezwe. Unausumbufu, changamano, na hautekelezeki au kukagulika.

ii. Tunapendekeza mfumo wenye ngazi mbili ambao utawezekana na kutambua matakwa ya jamii nay ale ya Idara ya wanyamapori.

- ***Malipo ya 1: Ada ya kitanda***
    - a. Ada hii itakubaliwa kati ya mwenye ardhi na mwekezaji (yaani kijiji/Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) au Idara ya Wanyamapori)
    - b. Mikataba inbaki kuwa halali
- ***Malipo ya 2: Ada ya shughuli za Wanyama***
    - a. Ada hii hulipwa kwa idara ya wanyamapori na pia hjumuisha mchango wa wilaya.
    - b. Ada hii itajumuisha shughuli za kiutalii zilizoorodheshwa katika upiga picha wa kitalii.
        - Utalii wa picha
        - Utalii wa picha -usiku
        - Safari za miguu
        - Milo nyikani
        - Mandari
        - Safari za mitumbwi
        - Ada ya kuongoza wageni

iii. Imependekezwa mfumo ufuatao wa ada (wasio wakJumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA)zi):

- Mapori ya Akiba $30
- Mapori tengefu $15
- Maeneo ya Wazi / Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) $10
- Ada hizi hazitahusika: Ada ya gari, Ada ya kuongoza wageni, Ada ya kundi, Ada ya kiwanja, Ada ya mtumbwi

iv. Uvuvi inafikiriwa ni shughuli ya uvunaji.

vi. Ada zisibadilishwe bila taarifa ya miezi 12.

vi. Makundi ya ada
- Wageni
- Wakazi
- Watu wazima
- Watoto na wanafunzi

vii. Ulinzi wa eneo

a. ada ya kitendo inweza kukusanywa na kulipwa kama kampuni ina makubaliano ya kulaza wageni na mwenye ardhi. Katika Mapori ya Akiba ada ya shughuli hupelekwa Idara ya Wanyamapori. Mapori Tengefu na Maeneo ya wazi ada ya shughuli hupelekwa kijijini.

b. Hii itadhibiti watalii wa mchana tu na uharibifu wa malihai, itahimiza ulinzi wa maliasili.

viii. Hitimisho

a. Ada zote zikokotolewe na kulipwa akaunti za benki idara ya wanyamapori au jamii tu
b. Malipo ya 1: malipo ya kitanda tayari yapo.
c. Malipo ya 2: Yataombewa kuanzia Julai 1 2008 na kulipwa moja kwa moja kwa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori
d. Lengo ni kuunda mfumo rahisi ambao ni rahisi kuusimamia, rahisi kuukagua, ulio wazi, unaojitosheleza, endelevu, unaohakikisha wote jamii na serikali kuu wanafaidika na unalinda maliasili kwa vizazi vijavyo.

***B. Mjadala wa jumla:***

Baada ya makundi kuwasilisha, ukumbi ulifunguliwa kuuliza maswali:

1. **Swali:** Je, mapendekezo haya yameelekezwa wapi? Je, tunajua ni kwa kiasi gani makampuni yananufaika kutokana na shughuli za kiutalii?
2. **Swali:** Je, si ada za viwanja ni kwa ajili ya makampuni yenye leseni za biashara tu? Kinachotakiwa ni ama ada ya kiwanja au ada ya utuaji ndege lakini sio vyote kwa pamoja.

   **Angalizo:** Washiriki walikuwa na mawazo kuwa ada ya kiwanja ingelipwa mara moja tu kwa mwenye kumiliki kiwanja, na pia kwamba ada ya kiwanja haiku chini ya Idara ya Wanyamapori, bali chini ya Mamlaka ya Anga.
3. **Swali:** Juu ya ada ya gari, kama uzito ndio suala, kwanini magari mengine ya kibiashara yasitozwe?
4. **Swali:** Je tunaweza kulundika ada zote pamoja ili kurahisisha mfumo?

   **Jibu kutoka kwa Mkurugenzi:** Dola 25,000 (USD) ni za ada ya uhifadhi, hata kama una miliki ardhi, kwa sababu wanyamapori ni mali ya umma.

### 3.6.2 Mawasilisho 2: Ni vipi watumiaji wa raslimali wanyamapori wanaweza kukaa pamoja?

***A. Mapendekezo:***

a. Wawekezaji wa utalii wa picha na uwindaji wanapaswa kufanya kazi kwa mwafaka.

b. Chombo cha uratibu wa utalii wa picha na matumizi yasiyo ya uvunaji ni budi kiundwe ili kuhusisha makampuni yote ya utalii katika maamuzi.

c. Wanavijiji, Maeneo ya hifadhi ya vijiji na wawekezaji ni vizuri wawe wazi kwa masuala ya mchakato wa zabuni mikataba, majadiliano na makubaliano ya kimikataba.

d. Mikataba katika maeneo ya Hifadhi ya Jamii yanatakiwa kupanda hadi kuwa miaka 5 na mteja apewe nafasi ya kwanza katika kufanya upya mkataba kama ametimiza vigezo husika kiutendaji.

e. Hamasa ya wadau wa utalii ni vema iinuliwe hasa katika sera, sheria, kanuni na misingi ya biashara.

***B. Mjadala wa Jumla:***

Baada ya mawasilisho ya vikundi, ukumbi ulifunguliwa kwa mjadala:

1. **Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori:** Kumbuka uwezekano wa kutenga kanda za matumizi kwa msimu au majira.
2. **Maoni kutoka vikundi:** Vyombo vya kuunganisha makampuni ya wapiga picha lazima viundwe, sio kuwa na chombo kimoja kitaifa. Utatuzi wa masual ngazi hii ni muhimu kwa sababau hali hutofautiana. Vyombo hivi mahususi vyaweza kuwa karibu sana na vitalu vya uwindaji. Kwa uratibu wa ngazi ya kitaifa, faida zake ni kwamba unaweza kuhusisha makampuni mengi zaidi kama ya ndege na mahoteli sio tu wawindaji na makampuni ya utalii wa picha.

   **Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori:** Wadau wa kutoka katika jamii lazima wahusishwe katika vyombo muhimu kama vile wakulima, wafugaji, watumiaji wa asili, na pia watafiti. Makampuni yasihalifu mipango ya usimamizi au matumizi ya ardhi ya Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA). Nani ataanzisha vyombo hivyo na nini itakuwa mchango wa serikali za mitaa?

***Maoni ya Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori: Ni tukio la kihistoria kuwa na makampuni ya wawindaji na makampuni ya utalii wa picha kwa pamoja.***

### 3.6.3 Mawasilisho 3: Ugawanaji Mafao na Mapato

***A. Mapendekezo:***

i. Makundi husika:
   - Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA)
   - Wilaya
   - Serikali kuu, Idara ya wanyamapori
   - Jamii

ii. Maeneo:
   - Maeneo ya Hiadhi ya Jamii
   - Mapori tengefu
   - Maeneo ya wazi
   - Mapori ya Akiba

iii. Mapendekezo ya Mgawanyo:

   a. Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA) – Uvunaji(Nyara) na Matumizi yasiyo ya uvunaji
      - Jamii 55 asilimia

- Wilaya 15 asilimia
- Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) 10 asilimia
- Idara ya wanyamapori 20 asilimia

b. Mapori Tengefu na Maeneo ya wazi – Uvunaji (Nyara) na matumizi yasiyo ya uvunaji
- Jamii 65 asilimia
- Wilaya 15 asilimia
- Idara wanyamapori 20 asilimia

c. Mapori ya Akiba Haikujadiliwa.

***B. Mjadala wa Jumla:***
Hakukuwa na makubaliano halisi kutoka mapendekezo ya kikundi.

**Angalizo la Sekretariet ya TNRF:** Mgawanyo wa mapato mara tu ukipokelewa toka Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) kama inavyoelezwa katika Kifungu cha 73 (2) ya Kanuni za Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA). Inasema "Jumuia ya kijamii iliyoidhinishwa (AA) itatakiwa kuhakikisha kuwa katika mapato yake ya mwaka inatenga:

**(a)** Si chini ya 15% ya mapato irudishwe katika kuendeleza raslimali;
**(b)** Si chini ya 50% ya mapato ipelekwe katika vijiji wanachama wanounda Maeneo ya Hifadhi za Wanyamapori za Jumuia (WMA);
**(c)** Si chini ya 25% ya mapato itumike kuimarisha Jumuia za kijamii ziliyoidhinishwa"

